## SIKU YA UKIMWI DUNIANI 2025:

# Kuvunja vikwazo vya kifedha, kuimarisha mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI




**Na Mohammed Sharksy, SUZA**

KILA mwaka inapowadia tarehe 1 Desemba, dunia hukusanyika kwa pamoja kuadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani. Ni siku ya kujikumbusha safari ndefu ya mapambano dhidi ya VVU, kuwaheshimu waliopoteza maisha, kutambua mafanikio yaliyopatikana, na kuamsha dhamira mpya ya kuutokomeza ugonjwa huu. Hapa Zanzibar, maadhimisho ya mwaka 2025 yanatarajiwa kufanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil, Mnazimmoja, na mgeni rasmi anarajiwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla.

Maadhimisho ya mwaka huu yanakuja wakati mataifa duniani kote yakiendeleza juhudi za kubuni mbinu mpya za kupunguza maambukizi na kuimarisha huduma za kinga na matibabu. Hali hii imeelezwa kwa kina na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya UKIMWI Zanzibar, Dkt Ahmed Mohamed Khatib, maarufu kama Dkt Benga, katika mahojiano maalum ya simu yaliyolenga kuchambua mwenendo wa Zanzibar katika mwitikio wa VVU/UKIMWI.

### Kaulimbiu ya Dunia na Mwelekeo wa Kitaifa

Kwa mwaka 2025, dunia imekubaliana na kaulimbiu inayosema Kuvunja Changamoto: Kubadilisha Namna Tunavyokabiliana na VVU/UKIMWI. Kaulimbiu hii inaakisi mwamko wa kimataifa wa kuvunja vizingiti vinavyowazuia watu kupata huduma za kinga, matunzo, na tiba. Dunia inabadilika kwa kasi, na hivyo hatua, mikakati, na mifumo ya kutoa huduma za VVU nayo lazima iendane na mabadiliko hayo. Inaweka uzito katika uwekezaji wa ndani, matumizi ya teknolojia, ushirikiano mpana, na mbinu bunifu katika utoaji wa huduma.

Tanzania, kupitia TACAIDS na Wizara ya Afya, imechukua mwelekeo unaosisitiza kwamba mapambano dhidi ya VVU ni jukumu la watu wote. Jamii inahimizwa kupata elimu sahihi, kupima afya, kutafuta huduma mapema, na kuchukua hatua za kuwalinda walioko katika hatari kubwa.

Kwa upande wa Zanzibar, kaulimbiu mahsusi ya mwaka 2025 ni Kuvunja Vikwazo vya Kifedha, Kuimarisha Mwitikio wa VVU/UKIMWI. Dkt Benga anaeleza kuwa ujumbe huu unasisitiza haja ya kuongeza rasilimali za ndani, kupunguza utegemezi kwa wadau wa nje, na kuweka nguvu zaidi katika kinga, tiba, elimu kwa jamii, na programu jumuishi za afya.

### Hali ya VVU/Ukimwi Duniani

Takwimu za UNAIDS kwa miaka 2024 na 2025 zinaonyesha mwanga mpya katika mapambano ya dunia dhidi ya VVU. Mafanikio makubwa yamepatikana katika kupunguza maambukizi mapya, kuongeza upatikanaji wa dawa za ARV, na kuboresha mifumo ya afya. Hata hivyo, bado dunia ina mzigo wa mamilioni ya watu wanaoishi na VVU, huku maelfu wakipata maambukizi mapya kila mwaka na mamia ya maelfu wakipoteza maisha kutokana na magonjwa yanayohusiana na UKIMWI.

Licha ya mafanikio makubwa ya upatikanaji mpana wa dawa za ARV, safari ya kufikia lengo la dunia la kumaliza UKIMWI ifikapo mwaka 2030 bado haijafika mwisho. Hali hii inaonyesha kuwa ulimwengu unahitaji kuimarisha ubunifu, uwekezaji, na ushirikiano ili kuwafikia wale waliobaki nyuma, hasa jamii zilizo katika mazingira hatarishi.

Mafanikio ya Tanzania katika Mwitikio wa VVU Tanzania imeendelea kuwa mfano mzuri wa mafanikio ya kiafya katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kupitia TACAIDS na Wizara ya Afya, huduma za upimaji, ushauri, na tiba zimepanuliwa na kuboreshwa. Kiwango cha maambukizi katika jamii kimeendelea kuwa katika wastani unaoweza kudhibitika, huku idadi kubwa ya watu wanaoishi na VVU wakijua hali zao.

Utoaji wa dawa za ARV umeimarika zaidi, na walio katika tiba wameonyesha viwango vya juu vya kudhibiti virusi mwilini. Haya yote yanaifanya Tanzania kuwa karibu zaidi na malengo ya kimataifa ya kuhakikisha UKIMWI hauwi tena tishio la afya ya umma.

Zanzibar miongoni mwa nchi zenye maambukizi machache zaidi Afrika Mashariki

Katika mahojiano hayo, Dkt Benga ameeleza kuwa Zanzibar imefanikiwa kudhibiti maambukizi ya VVU na kubaki na kiwango cha chini kabisa ukilinganishwa na mataifa mengi ya Afrika Mashariki. Takwimu za mwaka 2025 zinaonyesha kuwa ni sehemu ndogo tu ya wananchi wanaoishi na VVU. Wengi wao tayari wako katika tiba na wanaendelea vizuri, jambo linaloonyesha ufanisi mkubwa wa mfumo wa huduma, ufuasi mzuri wa tiba, na uongozi dhabiti katika sekta ya afya.

Mafanikio haya yanatokana na mchanganyiko wa mambo kadhaa, yakiwemo uongozi imara wa serikali, ushirikishwaji wa jamii katika elimu na kinga, pamoja na uwekezaji endelevu katika huduma shirikishi zinazojumuisha ushauri, upimaji, na matibabu.

### Makundi Yaliyo katika Hatari Zaidi

Ingawa kiwango cha maambukizi Zanzibar ni cha chini, bado baadhi ya makundi yanabeba mzigo mkubwa wa maambukizi. Dkt Benga anabainisha kuwa watu wenye umri wa miaka 45 na zaidi wanaonekana kuathirika zaidi, huku wanawake wakibeba mzigo mkubwa kuliko wanaume.

Makundi muhimu kama wafanyakazi wa ngono, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, na watu wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya sindano, yanaendelea kukabiliwa na changamoto zinazoongeza hatari ya maambukizi. Makundi haya yanahitaji huduma za heshima, usalama, na uelewa wa kimazingira bila ubaguzi.

### Changamoto zinazoendelea kuwapo

Katika uchambuzi wake, Dkt Benga ametaja changamoto zinazotishia kasi ya mafanikio yaliyopo. Uelewa mdogo kwa vijana kuhusu kinga na huduma za VVU unaendelea kuwafanya wawe katika hatari zaidi ya kupata maambukizi. Vijana wengi hawana taarifa sahihi kuhusu upimaji, tiba, au namna ya kujikinga, hali inayoongeza mwanya wa maambukizi mapya.

Kupungua kwa ufadhili wa wahisani ni changamoto kubwa inayoikabili Zanzibar na mataifa mengi ya Afrika. Msaada wa kifedha kutoka kwa washirika wa maendeleo umekuwa ukipungua taratibu, hivyo kuifanya safari ya kuhakikisha huduma endelevu za VVU kuwa ngumu zaidi endapo rasilimali za ndani hazitaongezwa.

Dkt Benga anasisitiza umuhimu wa kuunganisha huduma za UKIMWI na huduma nyingine za afya kama afya ya uzazi, huduma za wajawazito, kifua kikuu, na msaada wa kisaikolojia ili kuimarisha mfumo mzima wa utoaji huduma. Pia unyanyapaa na ubaguzi bado ni kikwazo kinachowazuia watu wengi, hasa makundi muhimu, kutafuta huduma kwa wakati

### Dhamira ya Serikali: Hatua na Mwelekeo Mpya

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia TACAIDS na Serikali ya Zanzibar kupitia ZAC zimeonyesha msimamo thabiti wa kuendeleza mapambano dhidi ya VVU. Uongozi unakusudia kuimarisha elimu ya jamii, kupanua upatikanaji wa upimaji na ushauri, kuongeza kasi ya huduma shirikishi za afya, kuhakikisha upatikanaji wa dawa za ARV bila kukwama, na kupambana na unyanyapaa katika maeneo yote ya jamii.

Mwelekeo huu unalenga kulinda hatua zilizofikiwa na kuongeza kasi ya safari kuelekea kizazi kisicho na maambukizi mapya ya VVU.

### Mwito wa Siku ya UKIMWI Duniani 2025

Maadhimisho ya mwaka 2025 yanatoa ujumbe wa kukumbusha kuwa safari ya kumaliza UKIMWI bado inaendelea. Dunia inapaswa kujiimarisha katika mikakati, kuwekeza katika teknolojia na utafiti, na kujenga mshikamano wa kijamii. VVU bado ni tishio kwa familia, uchumi, afya, na maendeleo ya nchi.

Mustakabali wa dunia isiyo na maambukizi mapya, isiyopoteza maisha kutokana na UKIMWI, na isiyonyanyapaa mtu yeyote uko ndani ya uwezo wetu. Kufikia malengo haya kunahitaji umoja, uamuzi, na uwajibikaji wa pamoja kutoka kwa jamii nzima.

Ikiwa tutachukua hatua leo, tukiwa wamoja kama taifa na dunia, tutajenga kizazi chenye afya, chenye matumaini, na chenye nguvu ya kuishi bila hofu ya VVU.